

OFISI YA RAIS - TAMISEMI



HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO



SHULE YA SEKONDARI HOLILI

SIMU:0766098531, 0784603949, 0769376005

S. L. P 8861,

MOSHI.

TAREHE

15/12/2020

Kumb.....

MZAZI/MLEZI WA

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2020

1. UTANGULIZI

Ninayo furaha kukuarifu kuwa mwanaoamechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka 2021 katika Shule ya Sekondari Holili. Shule ya sekondari Holili ipo umbali wa mita 600 kutoka stendi ya Daladala Holili Mjini.

Ushirikiano wako na wafanyakazi wote pamoja na wanafunzi wenzako ni siri kubwa ya mafanikio. Hii inawezekana ukiwa na NIDHAMU, JUHUDI na MAARIFA. Ukiwa hapa shuleni utakuwa na wajibu mkubwa wa kusoma kwa bidii, kufuata sheria za shule, kushiriki katika mipango ya elimu ya kujitegemea na kufuata taratibu zote za shule zitakazotolewa na viongozi wako shuleni. HILI LIWE NDILO LENGO LAKO UTAKAPOKUWA SHULENI

Shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021**.Unatakiwa kufika shuleni siku hiyo bila kukosa. Mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe 29/01/2021. Iwapo hutarioti hadi tarehe hiyo utahesabiwa kuwa umekataa nafasi uliyopewa, hivyo nafasi itahesabiwa kuwa wazi na itajazwa kwa kufuata taratibu za uchaguzi wa wanafunzi wanaochaguliwa kujiunga na shule za serikali.

KARIBU SANA HOLILI SEKONDARI

MOTTO: "DISCIPLINE, EDUCATION AND WORK"

EMANUEL THADAYO

KAIMU MKUU WA SHULE



Edit with WPS Office

2. MAHITAJI YA MWANAFUNZI

a) SARE ZA SHULE

• WAVULANA

- (i) Suruali mbili za rangi ya **kaki** (original) (tazama kitambaa iliyobandikwa kwenye fomu hii) zisizobana zenyne upana wa inchi 17 chini, marinda mawili kila upande kwa mbele, mifuko ya mbele iwe miwili (mmoja kila upande) na isiwe kama ya suruali ya jeans, isiwe ya kubana/chupa. Mfuko wa nyuma mmoja (uwe upande wa kulia na usiwe wa kubandika). Pindo za chini za suruali zikunjwe kwa nje (iwe na "turn up"). Tunashauri suruali ya kushona ndio nzuri kuliko ya mtumba/dukani (**asiyefuata maagizo haya hatapokelewa**)
- (ii) Mashati mawili meupe yenyne mikono mifupi. Nguo itakayovaliwa ndani ya shati iwe **nyeupe** mfano 'vest' au 'singlet'.
- (iii) Viatu vya ngozi vyeusi jozi mbili vya kufunga kwa Kamba. Visiwe na soli nene/kisigino kirefu na hairuhisiwi kuvalaa viatu vya matairi, kandambili au yeboyebo wakati wa masomo darasani. (**lizingatiwe**).
- (iv) Soksi jozi mbili rangi **nyeusisi** (plain black), ndefu, isiyo na urembo wowote.
- (v) Sweta moja la muundo wa "**V**" rangi ya kaki (original)
- (vi) Mkanda **mweusisi** (Jozi mbili), na usiwe na urembo wowote. Sehemu ya kufungia isiwe na chuma kinene kupita kiasi (uwe wa heshima/ usivae mkanda wa begi).
- (vii) Tai mbili ndefu za rangi ya kaki

• WASICHANA

- (i) Sketi (2) za rangi ya kaki (original) (tazama kitambaa iliyobandikwa kwenye fomu hii), mshono wa mapindo nane (8), **ndefu hadi kwenye viatu**
- (ii) Shati (2) nyeupe mikono mifupi lenye mfuko mmoja kifuani upande wa kushoto lisilobana mwili na urefu wa kutosha kuchomekeea. Nguo itakayovaliwa ndani ya shati iwe nyeupe mfano vest au singlet.
- (iii) Viatu vya ngozi vyeusi (jozi mbili) viwe vya kufunga na kamba na visiwe vinapiga kelele, viwe vinafunika kabisa (visiwe vya wazi) na visiwe na kisigino kirefu.
- (iv) Soksi nyeupe ndefu (Stocking) sio za kuonyesha mwili.
- (v) Sweta lifanane na rangi ya sketi. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na sweta hasa ukizingatia kuna msimu wa baridi kali na msimu wa mvua. Hivyo kuwa na sweta ni hiari ila ni **marufuku** kuvalaa aina nyingine ya sweta/koti/jaketi tofauti na sare ya shule. **N:B** mwanafunzi akikamatwa na nguo za nyumbani hatarudishiwa na atapewa adhabu kali.
- (vi) Hijabu na nusu kanzu zitavaliwa na wasichana waislamu tu wanaopenda (Hijabu rangi yake iwe nyeupe, ifike kiunoni na isiyo na urembo na **nusu kanzu** iwe nyeupe na ifike kwenye nyonga).

3. VIFAA VYA TAALUMA

Mwanafunzi anahitajika kuja na vifaa vifuatavyo pindi atakapo ripoti shulenii kwa ajili ya kujifunza:-

- (i) Daftari kubwa (counter books - 2 quire au 3) ziwe kumi (10)



Edit with WPS Office

- (ii) Peni (kalamu zisizopungua 2 au zaidi), Penseli na mfutio
- (iii) Mkebe wa hesabu (Mathematical set) moja (1)
- (iv) Daftari ndogo tisa (9) kwa ajili ya majoribio ya kila wiki
- (v) Rula moja (1) yenyе sm 30
- (vi) Passport size (picha) zenyе rangi ya bluu nyuma nne (4)
- (vii) Kitambulisho na nembo ya shule sh.5000/-
- (viii) Faili (folder file) moja (1) kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu zake
- (ix) Rimu moja (1) kwa ajili ya kufanya mitihani shuleni
- (x) Kamusi ya Kiswahili sanifu moja (1) - yake mwenyewe atakayotumia

4. VIFAA VINGINE VYA KUFANYIA USAFI

- (i) Wavulana – walete jembe
- (ii) Wasichana – walete ndoo moja (1) kubwa ya lita 20 na ufagio wa chelewa
- (iii) Sahani 1, bakuli 1, kikombe (vyote vya chuma) na kijiko kwa ajili ya chakula

5. MAHITAJI MENGINE YA KIBINADAMU

Michango ya chakula na maendeleo ya shule itatokana na makubaliano ya kikao cha wazazi kama inavyoiezwa katika waraka wa Elimu namba 3 wa mwaka 2016.

6. FOMU MBALIMBALI KWA MZAZI/MLEZI/MWANAFUNZI ZA KUJAZA

Fomu mbalimbali za kujazwa na mwanafunzi/ mzazi/mlezi ziambatanishwe.

N:B, Hakikisha unamfanya vipimo mwanafunzi katika hospitali ya serikali kwa kutumia fomu iliyambatanishwa na uwasilishе risiti ya upimaji kutoka katika kituo au hospitali ya serikali siku anayoripoti shuleni. **NI LAZIMA**



Fomu Na – A
SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya RAISI – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu.

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

1. Mwanafunzi anapaswa kuwepo eneo la shule wakati wote isipokuwa anapopata ruhusa maalum kutoka kwa mwalimu wa zamu, Makamu Mkuu wa Shule au Mkuu wa Shule
2. Mwanafunzi anatakiwa kucaa sare rasmi ya shule muda wote wa shule, isipokuwa muda wa michezo ambapo atavaa nguo rasmi za michezo
3. Lugha chafu, matusi, ugomvi, fitina na kupigana kwa mwanafunzi ni marufuku
4. Mwanafunzi lazima awahi popote anapotakiwa na wakati uliowekwa
5. Mwanafunzi ni lazima aiheshimu kazi ya darasani na nje na kuifanya vizuri. Ni lazima kufanya mazoezi ya mitihani yote inayotolewa darasani awapo shulenii
6. Unywaji wa vileo, kuuza pombe na uvutaji wa aina yoyote ya sigara au madawa ya kulevyia ni marufuku kwa mwanafunzi. Hairuhusiwi kufanya biashara yoyote shulenii
7. Wizi wa aina yoyote ni marufuku na ni kosa kubwa kwa mwanafunzi
8. Uharibifu na upotevu wa mali binafsi au ya Umma ni kosa kubwa
9. Mwanafunzi anapaswa kuwa na heshima, mtiifu na mwenye adabu wakati wote na kwa kila mtu. Ukaidi na ubishi kwa viongozi/walezi wake ni kosa
10. Ni marufuku kuwa na mahusiano ya kimapenzi uwapo shulenii. Akibainika atafukuzwa shule mara moja
11. Ni marufuku kwa wanafunzi kwenda nyumba za Walimu na Wafanyakazi wasio walimu bila ruhusa au kibali maalum toka kwa Mwalimu mlezi/Uongozi wa shule.
12. Mapambo na nakshi za aina yoyote na mavazi ya kihuni kwa mwanafunzi ni marufuku, nywele ziwe fupi, ndeu ni marufuku. Mitindo ya kunyoa nywele kama pank, kunyoa kipara pasipo sababu hatutavumilia na adhabu kali itatolewa kwa atakayefanya kinyume na haya (Aidha kofia aina yoyote, mikanda mipana na majaketi marufuku kabisa shulenii)
13. Simu haziruhusiwi na ukikamatwa utapewa adhabu kali na simu hiyo hutarudishiwa tena.
14. Ni marufuku kwa mwanafunzi kukataa/kugomea adhabu kwani kukataa adhabu ni kukataa malezi bora ya walezi wako shulenii yenye maana ya kukataa kuwa mwanafunzi wa shule hii
15. Mgomo wa aina yoyote ni marufuku na ni haramu kwa mujibu wa sheria za nchi ya Tanzania. Matatizo yote yatashughulikiwa kwa kufuata ngazi zilizowekwa. Atakayegoma au kusababisha mgomo adhabu yake ni kufukuzwa shule

MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA MASOMO AU SHULE

1. Wizi, Kuoa, kupata mimba/kusababisha mimba, Uasherati, Ushoga, mahusiano ya kimapenzi, Ubakaji na kupiga/kupigana
2. Ulevi, Uvutaji wa bangi na sigara ikiwa ni pamoja na madawa ya kulevyia
3. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma /binafsi
4. Kudharau wimbo wa Taifa, wimbo wa Shule na Bendera ya Taifa
5. Kugoma, kuchochea au kuongoza mgomo, ikiwa ni pamoja na kukataa adhabu kwa makusudi ikiwemo kuvuruga amani na usalama wa shule




6. Kunyanyapaa au Uonevu wa aina yoyote kwa mwanafunzi mwenzake
7. Kufanya mikutano isiyoko halali au isiyokuwa na kibali kutoka uongozi wa shule
8. Kuharibu miundombinu na samani za shule kama viti, meza, umeme, maji kwa makusudi
9. Utoro Zaidi ya siku 84 bila taarifa
10. Kuwa na simu ya mkononi

..... JINA LA MWANAFUNZI

..... SAHIHI

..... TAREHE.....

EMANUELTHADAYO



..... KAIMU MKUU WA SHULE



Edit with WPS Office

Fomu Na -B-
TAARIFA MUHIMU ZA MWANAFUNZI

Shule inapenda kupata taarifa muhimu za kila mwanafunzi kwa ajili ya mawasiliano wakati wote awapo shulenii. Fomu hii ijazwe kwa usahihi na ukamilifu.

Jina la mwanafunzi (majina matatu)

Anwani ya nyumbani (anayotumia).....

Tarehe ya kuzaliwa.....

Namba ya simu (ya nyumbani/ya mzazi)

Mtaa/Kijiji anachotoka..... Kata..... Tarafa.....

Wilaya..... Mkoa..... shule ya msingi aliyosoma.....

AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi..... NAKUBALI/SIKUBALI nafasi niliyopeLAZIMA

ika shule ya sekondari Holili. Naahidi kuwa nitazitii taratibu, kanuni na sheria zote za shule. Nitafuata masharti yote yanayotolewa na Mkuu wa shule, Wafanyakazi wote na Viongozi wote wa shule. Ninaahidi pia nitashirikiana na wanafunzi wenzangu katika shughuli za masomo, kazi za nje na katika michezo kwa muda wote nitakaokaa Holili Sekondari. Nakiri kuwa kwa akili zangu timamu, taarifa zote nilizotoa hapo juu ni sahihi na zinanihusu.

Jina sahihi Tarehe

TAARIFA YA MZAZI/ MLEZI

Jina la Mzazi/Mlezi

Anwani yake.....

Namba ya simu

Kazi anayofanya

Wilaya/Mji anakofanya kazi.....

AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi..... MZAZI/MLEZI NAKUBALI / SIKUBALI nafasi aliopewa mwanangu katika shule ya sekondari Holili. Naahidi kuwa nitawajibika/sitawajibika na kumhimiza mwanangu kuzitii taratibu, kanuni na sheria zote za shule. Nitashiriki/sitashiriki kumhimiza kufuata masharti yote yanayotolewa na Mkuu wa shule, wafanyakazi wote na viongozi wote wa shule. Ninaahidi pia nitashirikiana/sitashirikiana na uongozi wa shule kumhimiza mwanangu kushirikiana na wanafunzi wenzake katika shughuli za masomo, kazi za nje na katika michezo na kuwa na nidhamu kwa muda wote atakaokaa Holili Sekondari. Nitapenda/sitapenda kupata taarifa zote zinazomhusu mwanangu muda wote awapo shulenii (**futa isiyohusika**)

Jina la mzazi/mlezi.....Sahihi.....Tarehe.....

WATU WA KARIBU (KIUHUSIANO/UNDUGU) NA FAMILIA AMBAO UNGEPENDA WAPATE
TAARIFA ZAKO ZAIDI YA WAZAZI/ WALEZI

- (i) Jina (majina matatu)
- (ii) Anwani
- (iii) Namba ya simu.....
- (iv) Kazi anayofanya
- (v) Uhushiano wake na mwanafunzi.....

NB: Iwapo anwani ya mmojawapo wa Mzazi/Mlezi au ndugu wa karibu amehama au Amefariki lazima mwanafunzi atoe taarifa na kubadilisha jina na kuandika mtu mwininge ambaye atawajibika kwa mwanafunzi



FOMU HII IJAZWE NA MGANGA MKUU WA MKOA /WILAYA NA MWANAFUNZI AJE NAYO
SHULENI NA KUIKABIDHI KWA MKUU WA SHULE

Mimi (Jina la Mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali)..... ninathibitisha kuwa
mwanafunzi huyu (Jina la mwanafunzi)..... amepimwa na mimi kikamilifu na
kuonekana kuwa anayo /hana afya nzuri kwa mujibu wa taarifa zifuatazo:-

(A) Hali ya Mwili

- (i) Mapigo ya moyo.....
- (ii) Damu (Haemoglobin).....
- (iii) Kundi la Damu (Blood group)
- (iv) Mkojo.....
- (v) Haja kubwa.....
- (vi) Macho.....
- (vii) Masikio

NB. Weka maoni yako kuhusu kile kilichotajwa

(B) Magonjwa

Amewahi /hajawahi au hana magonjwa yafuatayo:-

- (a) Kifua kikuu (TB).....
- (b) Kifafa (Epilepsy).....
- (c) Shinikizo la damu (BP).....
- (d) Magonjwa ya tumbo
- (e) Seli mundu (Sickle cells).....
- (f) Ukoma.....
- (g) Magonjwa ya zinaa (taja aina)
- (h) Ugonjwa wa akili
- (i) Ugonjwa mwingine nje ya orodha hapo juu

Maoni ya Daktari

Saini na Muhuri wa Daktari/Mganga wa Hospitali ya Serikali

